MASWALI

Kusikiliza na kuzungumza

A. Imla

Mwanafunzi asomewe maneno kisha ayaandike kwenye mapengo.

Maneno ya Imla

1. Bwana
2. fyonza
3. mwanafunzi
4. kwama
5. fyatuka
6. Nyundo
7. mwewe
8. kimbilia
9. ndimu
10. ukabila
11. chinja
12. pwaguzi
13. vyombo
14. kuteketea
15. vifaa

B Soma maneno haya kwa sauti alikwea

bweni	alikwea	fyeka	afya
mbegu	aliomba	vunjika	njama
mzalendo	kwekwe	pwaya	daktari
shuka	mchoro	hamali	

C. Soma sentensi hizi kwa sauti

1. Kwa nini njiwa wamelala?
2. Wewe hukuimba wimbo wa taifa.
3. Nyinyi mlisafisha mazingira.
4. Walimu walitufunza tabia nzuri.
5. Usikae na mtu usiyemjua.
6. Salama alizaliwa mwezi wa Machi.

D. UFAHAMU

Mzazi au mlezi amsomee mwanafunzi taarifa hii kwa sauti mara mbili kisha amwulize maswali.

Shule zilipofungwa kwa likizo ya Aprill sikukaa tena mjini. Nilifunga safari yangu hadi mashambani kwa shangazi yangu. Shangazi yangu ni mkulima maarufu katika kijiji cha kwao. Nilifika kwa shangazi alasiri. Shangazi na watoto wake walikuwa shambani wakilima. Nilienda hadi shambani na nikaanza kulima. Hata sikubadilisha nguo.

Jioni tulienda nyumbani. Shangazi alipika kilalio. Baada ya kula, sisi sote tulienda kulala. Mimi nililala katika kitanda kimoja na mkoi wangu. Niliomba Mungu sana usiku huo nisikojoe kitandani; sikutaka kuchekwa na wakoi wangu.

Maswali

1. Shule zilipofungwa mwandishi aliondoka wapi? .....